



Matumizi sahihi ya vifaakinga wakati wa kupulizia viuatilifu kwenye mimea.

HATUA ZAIDI ZA KUENDELEZA KINGA BAADA YA MUHOGO KUCHIPUA

Endelea kukinga muhogo shambani hadi kufikia miezi minne au mitano kwa kupulizia mchanganyiko wa viuatilifu aina ya Imidacloprid na Deltamethrin kwa utaratibu ufuateo:

❖ Pulizia mchanganyiko huo kati ya mwezi wa kwanza na wa tano baada ya muhogo kuchipua.

Jinsi ya kuchanganya na kupulizia viuatilifu

❖ Changanya mililita 20 za kila kiuatilifu kwenye lita 10 za maji safi ndani ya bomba.

❖ Pulizia mchanganyiko huo kwenye muhogo hadi matone yachuruzike kwenye majani.

FAIDA ZA KUKINGA VIPANDO VYA MUHOGO KWA KUTUMIA VIUATILIFU

- ❖ Hukinga vipando dhidi ya visumbufu vya aina nyingi kwa mfano: nzi mweupe, vidugamba, vidung'ata, mchwa na sondo wa mbawakavu.
- ❖ Huharakisha uchipuaji wa vipando.
- ❖ Huzuia kuenea kwa virusi vya magonjwa ya batobato na michirizi ya kahawia.

HITIMISHO

Uthibiti husishi wa nzi mweupe wa muhogo ni muhimu ili kuzuia visumbufu vya mimea kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kipato katika familia.

WADAU



Mawasiliano: Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Mikocheni, simu 22 2700552, Barabara ya Coca Cola,

kitalu Na.22, Dar es Salaam, Email: cmmikocheni@tari.go.tz / www.tari.go.tz



UDHIBITI HUSISHI WA NZI MWEUPE WA MUHOGO



Nzi mweupe wa muhogo

Nzi Mweupe wa Muhogo ni Nini?

Nzi mweupe wa muhogo ni mdudu mdogo ambaye husababisha madhara mengi kwenye zao la muhogo hivyo ni lazima adhibitiwe kwa kutumia mbinu za uthibiti husishi

Udhibiti Husishi ni Nini?

Udhibiti husishi ni matumizi ya mbinu mbalimbali za ku nzi mweupe kwa lengo la kupunguza uwezekano wa kutokea usungu dhidi ya viuatilifu vinapotumika.

❖ Kupanda aina ya muhogo yenye ukinzani dhidi ya nzi mweupe.

KUPANDA AINA YA MUHOGO YENYE UKINZANI DHIDI YA NZI MWEUPE

Baadhi ya mbegu za mihogo zime-fanyiwa utafiti na kubainika kuwa na ukinzani dhidi ya nzi mweupe. Aina hizo ni Mkumba na TARICASS 4 (TZ 130)




Muhogo aina ya TARICASS 4 (TZ 130)

KUTUMIA VIUATILIFU

Viuatilifu ni kemikali zinatotengenezwa viwandani ambazo hutumika katika kudhibiti visumbufu vya mazao.

Vipo viuatilifu vya aina nyingi vinavyoweza kutumika.

- ❖ Imidacloprid
- ❖ Deltamethrin



Kiuatilifu aina ya Imidacloprid



Kiuatilifu aina ya Deltamethrin

Kudhibiti nzi mweupe kwa kutumia viuatilifu kunaweza kukinga mbegu za mihogo dhidi ya mdudu huo hatari.

JINSI YA KUKINGA MBEGU ZA MUHOGO KWA KUTUMIA VIUATILIFU

HATUA ZA KUFUATA WAKATI WA KUTUMIA KIUATILIFU AINA YA IMIDACLOPRID

1. Chagua mbegu (vipando) kutoka kwenye mashina ya muhogo usiokuwa na dalili za batobato au michirizi ya kahawia.

2. Tayarisha vipando hivyo vya muhogo vyenye urefu kati ya sentimita 15 hadi 20 na kila ki-moja kiwe na macho matatu hadi matano.

3. Changanya mililita 20 za kiuatilifu kwenye lita 10 za maji safi ndani ya beseni, kisha koroga ili upate mchanganyiko mzuri. Tumbukiza vipando vilivyoandaliwa kwenye mchanganyiko huo.

4. Zamisha vipando kwenye mchanganyiko huo na vibaki humo kwa muda wa saa tatu hadi nne.

5). Toa vipando kwenye mchanganyiko huo na viweke kivulini kwa muda wa saa mbili hadi tatu ili vitoke unyevu.

KUMBUKA

Viuatilifu hivyo hupatikana katika maduka yote ya pembe-jeo za kilimo nchini.